

# Kuongeza Idadi ya Marafiki Wangu

Daftari hili litakusaidia (1) kuwatambua marafiki wako wa karibu na (2) kuona jinsi ya kuwahusisha wengine kwenye urafiki huo.


**Kwa nini ni muhimu?:** Kuwatenga watu wengine wasiwe marafiki wako wa karibu kunaweza kukunyima mambo mazuri ambayo ungepata ikiwa ungekuwa na uhusiano nao.

1

Kwenye duara ya ndani, andika majina ya marafiki wako wa karibu zaidi.

2

Kwenye duara ya nje, andika majina ya watu ambao ungependa kuwajua vizuri.



“Kuanzisha urafiki na watu wenye mapendezi na umri wako tu kunaweza kukufanya ukose urafiki wa watu wengi wenye umri tofauti na malezi tofauti na yako. Kunaweza hata kukufanya usijue jinsi unavyoweza kuboresha utu wako.”  
—Melinda.

## Ni nani ambaye ungependa kumjua vizuri?

Kwenye orodha hii, chagua sifa tatu ambazo ungependa rafiki yako awe nazo. Ikiwa unafikiri kwamba baadhi ya sifa hazikuandikwa katika orodha hii, ziandike kwenye nafasi zilizoachwa wazi.



Mnyoofu

Anategemeka

Anatunza Wakati

Mwenye Utaratibu

Ana Mtazamo Mzuri

Hana Ubaguzi

Mkarimu

Anafanya Kazi kwa Bidii

Anajizuia

.....

.....

Sasa orodhesha majina ya watu unaojua kwamba wanaonyesha sifa ulizochagua. *(Si lazima wawe na umri sawa na wako.)*

.....

.....

.....

.....

# MADHARA NA FAIDA



Ni madhara gani unayoweza kupata kwa kumfahamu mtu ambaye kwa sasa si mmoja wa marafiki wako?

.....  
.....  
.....



Unaweza kupata faida gani?

.....  
.....  
.....

## UNGEMPA USHAURI GANI?

“Mara nyingi ninajikuta nikizungumza na marafiki walewale wa karibu. Ingawa ninazungumza na wengine pia, lakini hatimaye ninarudi kwa marafiki walewale. Ninafikiri mara nyingi vijana wengine wana tatizo kama langu, wanaogopa hawatakubaliwa na mtu mwingine yeyote, kwa hiyo hawafanyi jitihada zozote za kuwajua watu wengine.”—Emily.

Ungempa Emily ushauri gani ili kumsaidia kushinda woga wa kutafuta marafiki wapya?

.....  
.....  
.....  
.....